# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI KWA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS SERA URATIB NA BARAZA LA WAWAKILISHI KUPITIA RIPOTI YA KAMATI YA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** kila sifa njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo ndani yake, kwa kutujaalia Uhai na Afya njema ambayo imetuwezesha kukutana tena katika Baraza hili Tukufu kwa lengo la kuwatumikia wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile, nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika pamoja na wasaidizi wako kwa kuliongoza vyema Baraza hili Tukufu kwa umahiri mkubwa na ninaamini kwamba mtaendelea kuliongoza kwa uadilifu wa hali ya juu zaidi ili kufikia malengo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi pamoja na Mipango na Mikakati mbali mbali ya Kitaifa katika kufikia hatua iliyobora kwa maslahi ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia, kuchukua fursa hii kumshukuru na

kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa uongozi wake uliotukuka ambapo ndani ya muda mfupi tu wa miaka miwili tumeona mambo aliyowafanyia wananchi wetu na kila mmoja ni shahidi katika mageuzi makubwa ya kiuchumi na kijamii. Kamati inaridhika sana na juhudi za Mheshimiwa Rais za kutembelea maeneo mbalimbali ya nchi yetu na kutatua matatizo ya wananchi. Aidha, uadilifu anaotuonesha unapelekea kupatikana kwa maendeleo ya kudumu mbali mbali kwa msingi ule ule wa kudumisha amani na utulivu wa Taifa hili. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kumpa hekma, busara na nguvu katika utumishi wake.

**Mheshimiwa Spika,** pia, sina budi kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratib na Baraza la Wawakilishi Mheshimiwa Hamza Hassan Juma kwa uweledi wake uliomfanya aweze kuteuliwa kuwa Waziri katika Ofisi hii pamoja na kuwapongeza watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Thabit Idarous Faina kwa mashirikiano yao wanayotupatia wakati wa shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, nitakuwa mchoyo wa fadhila iwapo sitowashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kwa umoja wao na uwezo wao, kwa hakika ni Wajumbe mahiri sana ambao wameweza kujadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali ambayo yametolewa ufafanuzi na Ofisi hii kwa lengo la kuhakikisha kwamba utekelezaji wa maagizo, maoni na ushauri uliotolewa ndani ya ripoti ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2021/2022 chini ya Taasisi zake, majibu yake yamekuwa ni sahihi na yanauhalisia katika utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na taadhima naomba sasa uniruhusu kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Zaina Abdulla Salum | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Mohamed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| *7.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *8.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *9.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati kwa kutumia Kanuni ya 107(3) inapewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia. Ambapo kazi hii ilifanywa vyema kwa kipindi hiki kilichopita na bado Kamati inazidi kufuatilia utekelezaji huo kila inapoona inafaa kufanya.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 108(14) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la 2020 imetoa fursa ya lazima kwa kila Kamati kutayarisha ripoti ya mwaka itakayowasilishwa katika kikao cha mwezi wa Februari cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hilo, Kanuni ya 108(15) ya Kanuni za Baraza, inaelezea kuwa kabla ya kuwasilishwa Barazani utekelezaji wa maoni na ushauri huo, Kamati inatakiwa kukaa na wizara husika kujadili utekelezaji huo.

**Mheshimiwa Spika,** ripoti hiyo hujumuisha ushauri na maoni ya Kamati kwa wizara na taasisi zake inazozifanyia kazi. Ambapo Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu inasimamia wizara tano (5) ambazo ni:

*(a)* Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera Uratib na Baraza la

Wawakilishi,

*(b)* Ofisi yaMakamo wa Kwanza wa Rais,
*(c)* Ofisi ya Rais,Ikulu,
*(d)* Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora;
*(e)* Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

**Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii inaelezea utekelezaji wa maoni na ushauri kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera Uratibu na Baraza la Wawakilishi.

**Utekelezaji wa Maagizo**

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Kamati yetu imeridhishwa sana na utekelezaji wa maoni na ushauri uliotolewa kupitia ripoti yetu ya mwaka jana, isipokuwa kutokana na changamoto mbali mbali zinazoikabili Wizara kupitia Taasisi zake zinazojitegemea Serikali ifanye mpango maalum wa kuzisaidia Taasisi hizi kuweza kujikwamua zenyewe kutokana na changamoto zao katika utekelezaji wa kila siku.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhishwa na kasi ya maendeleo ya Miradi ya TASAF katika kuendeleza juhudi za Serikali yetu tukufu za kunyanyua uchumi wa wananchi wanaoishi katika Mazingira magumu, kufuatia maoni na ushauri uliotolewa. Kamati yangu pia ilitaka ufafanuzi juu ya mpango wa upatikanaji wa miradi ya OPEC hapa Zanzibar na kuangalia namna gani miradi hii mikubwa kabisa inaweza kutekelezwa kwa lengo la kuwasaidia wananchi. Hata hivyo, miradi hii kwasasa haonekani kutekelezwa hapa Zanzibar kutokana na Sababu mbali mbali zenye mnasaba na masharti ya miradi ya OPEC. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kufuatilia kwa kina juu ya utekelezaji wa miradi hii kwani ni muhimu sana kwa maslahi ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia inaishauri Serikali kuandaa programu maalumu ambayo itawezesha kutunza na kuendeleza kumbukumbu za muasisi wa Taifa hili Marehemu Abeid Amani Karume Rais wa kwanza wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na muasisi wa Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964. Kamati imeona ni vyema Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kushirikiana na Ofisi ya Rais Ikulu kufanya juhudi maalum ya kuitunza nyumba ya marehemu iliyopo Mwera Wilaya ya Kati pamoja na kutunza sehemu moja ya vifaa mbali mbali ambavyo alikuwa akitumia katika uhai wake. Aidha kamati inashauri pia, Serikali kushirikiana kwa karibu na hifadhi ya makumbusho ya baba wa Taifa iliyopo Butiama, ili kuwajengea uwezo watumishi wataohusika na uwekaji wa kumbukumbu wa Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, Muasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kamati inashauri katika kusaidiwa na kuboreshwa utendaji wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar kuondolewa kwa fungu la Makusanyo ya fedha zinazopatikana katika uchukuaji wa fomu za uchaguzi kwa kuwa chanzo hiki hakina uhakika na huchukua muda mrefu bila ya makusanyo yoyote kupatikana.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia hotuba yangu, naomba kutoa shukrani za pekee ziende kwa Rais wetu mpendwa Mheshimiwa, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa namna alivyoleta mageuzi katika sekta mbali mbali za kimaendeleo. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuzidisha kasi ya maendeleo kwa wananchi ili kufikia malengo ya kupunguza umaskini katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa, napenda kuchukuwa fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni machache sana ya Kamati yangu, kwa niaba ya Kamati pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa

Baraza lako kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Naomba Kuwasilisha.

Ahsante,

……………….…………….

(Machano Othman Said)

***Mwenyekiti,***

***Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,***

BARAZA LA WAWAKILISHI,

ZANZIBAR